

## SIWATI

1. Siwati nishishiyelo, siwati kwani niwate?  
Siwati ni lilo hilo, 'talishika kwa vyovyote  
Siwati ni mimi nalo, hapano au popote  
Hadi kaburini sote, mimi nalo tufukiwe
2. Siwati ngaadhibiwa, adhabu kila mfano  
Siwati ningaambiwa, 'tapawa kila kinono  
Siwati lililo sawa, silibanduwi mkono  
Hata ningaumwa meno, mkono siubanduwi
3. Siwati si ushindani, mukasema nashindana  
Siwati ifahamuni, sababuye waungwana  
Siwati ndangu imani, niithaminiyo sana  
Nakuiwata naona, itakuwa ni muhali
4. Siwati nimeradhiwa, kufikwa na kila mawi  
Siwati ningaambiwa, niaminiyo hayawi  
Siwati kisha nikawa, kama nzi; hivyo siwi  
Hamma nakariri siwi, na Mn'gu nisaidiya

*Abdilatif Abdalla, "Bwana-wa-Mtambwe"  
Kidundo-uchawi  
15 Machi 1970*